# INTERNATIONAL STAR

# APRILI/ MEI

## KISWAHILI 2020

## SEHEMU YA KWANZA:

**LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO:**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.

2. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.

4. Hakikisha ya kwamba umeandika yafuatayo katika karatasi ya majibu:
   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.

6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.

7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.

8. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.

9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

   **Mfano:**
   **Katika kijitabu cha maswali:**
   **21.** 'Tunakimbiana' maana yake ni:
   A. Tunaogopana
   B. Tunahepana
   C. Tunasaidiana
   D. Tunachukiana

   Jibu sahihi ni B
   **Katika karatasi ya majibu:**

   1 [A] [B] [C] [D] 11 [A] [B] [C] [D] 21 [A] [B] [C] [D] 31 [A] [B] [C] [D] 41 [A] [B] [C] [D]

   Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **21**, kisanduku chenye herufi **B** ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.

11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

***Kamilisha kifungu kifuatacho kwa kutumia viteuzi ulivyopewa.***

Ufisadi ni utumiaji mbaya wa mali ya chama, shirika au serikali; yaani ______1_____ Vile vile ni utoaji na ____2_____wa ____3_____Tabia _____4____ huchangia sana ______5____ uchumi ______6____ nchi. Watu wengi siku hizi ______7______ili kufanyiwa mambo kwa mapendeleo. Tabia hii haina budi kuwahiwa mapema kabla ya______8_______ taifa kwani______9______.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. ukinaifu | B. ukorofi | C. ushirikina | D. ubadhirifu |
| **2.** | A. kupewa | B. upokeaji | C. kupokea | D. mapokezi |
| **3.** | A. fola | B.hiangazamacho | C. chirimiri | D. riba |
| **4.** | A. hii | B. hiyo | C.hilo | D. huo |
| **5.** | A. kuzorotesha | B.uzorotaji | C. kuzorota | D. kuimarisha |
| **6.** | A. ya | B. za | C. wa | D. na |
| **7.** | A. hupiga mbizi | B.hupiga vijembe | C. hulamwande | D. huzunguka mbuyu |
| **8.** | A. kuwaangamiza | B.kuliangamiza | C.kutuangamiza | D. kuiangamiza |
| **9.** | A. kikulacho ki nguoni mwako | B. usipoziba ufa utajenga ukuta | C. mwiba wa kujichoma huambiwi pole | D.maji mengi hayazuiliki |

Wanafunzi walielekea _____10_____na kuketi wakisubiri _______11_____ ya mwalimu mkuu sisi _____12_______tulimheshimu Bi Fatuma. Ilikuwa kawaida kama _____13______Kwake kukutana nasi kila sabato kujadiliana kuhusu mambo ______14______sisi vijana pale shuleni. Kwa njia hii tuliweza kudumisha _____15______mzuri baina ya wakufunzi kwa wanafunzi au walimu kwa wanafunzi.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | A. Ukumbini | B.Sebuleni | C. Handakini | D. Hamamuni |
| **11.** | A. Kumbukumbu | B.Mjadala | C. Ngano | D. Hotuba |
| **12.** | A. Zote | B.Wote | C. Sote | D. Yote |
| **13.** | A. Ibada | B.Sheria | C. Mauti | D. Ada |
| **14.** | A. Iliyotuathiri | B.Yaliyotuathirisha | C. Zilizotuathiri | D. Yaliyotuathiri |
| **15.** | A. Utengano | B.Utangamano | C. Utenguo | D. Utekelezaji |

**Kuanzia swali la 16 mpaka, 30 jibu kila swali kulinganana maagizo uliyopewa.**

**16.** Tambua kundi lenye vivumishi vya idadi isiyodhihirika kati ya ulivyopewa;

A. Nane, sita, kumi
B. Wengi, kadhaa, chache
C. Kwanza, wa tatu, wote
D. Mkubwa, nyingi, wanene

**17.** Chombo kipi hutumiwa kubania mbao zinapofanyiwa kazi?

A. Koleo
B. Fuawe
C. Jiriwa
D. Baro

**18**. Ni sentensi ipi yenye **"KWA"** ya kuonyesha sababu.

A. Alijibu kwa woga
B. Tulikula nyama kwa wali
C. Aliogopa kwa kukosa nguvu
D. Kukosa kwake nguvu kulitushtua

**19.** Kamilisha………………. nilifika mapema sikufanya chochote.

A. taraa
B. aghalabu
C. angalau
D. ijapokuwa

**20**. Tegua kitendawili kifuatacho. Hutafuna ila hamezi.

A. Ulimi
B. Mbuzi
C. Shoka
D. Mtoto

**21**. Andika hali ya kutendewa ya: Mwinyi alimletea Koko kikombe kizuri.

A. Kikombe kizuri kilitewa Koko na Mwinyi.

B. Koko aliletewa kikombe kizuri na Mwinyi.

C. Mwinyi aliletewa kikombe kizuri na Koko

D. Mwinyi na Koko walileteana vikombe vizuri.

**22.** Tambua sentensi yenye kielezi cha **wakati**

A. Shughuli zote zitakamilika Jumapili
B. Wimbo huo uliimbwa mara kadhaa
C. Mayatima wengi huteseka sana
D. Gari la abiria limeegeshwa pembeni

**23**. ………. ni kipande cha tatu katika ubeti wa shairi

A. Mloto
B. Ukwapi
C. Utao
D. Mwandamizi

**24**. Ipi si maana ya neno chupa?

A. Kifaa cha kutilia viowevu
B. Kitendo cha nguo kuwa ndefu
C. Kuruka kutoka juu hadi chini
D. Kuruka kutoka tawi hadi jingine

**25**. Neno gharama lina sauti ngapi ?

A. 4

B. 7

C. 6

D. 5

**26**. Msemo wenye maana ya kutupa kitu na kukisahau kabisa ni

A. Tupa jongoo na mti wake.
B. Kabili nyoka na mapindi yake
C. Valia miwani
D. Jitia hamnazo

**27**. Tambua ala ya muziki ya kizamani

A. Fidla
B. Zeze
C. Gitaa
D. Msondo

**28**. Unda sifa kutokana na kitenzi adili

A. Adili
B. Vadili
C. Adilifu
D. Uadilifu

**29**. Tambua methali isiyo na maana sawa na nyingine

A. Bidii ya mja haiondoi kudura
B. Mtaka cha mvunguni sharti ainame
C. Ukitaka la waridi sharfi udhurike
D. Bidii hulipa

**30**. Kati ya mapambo yafuatayo ni lipi si la kichwani?

A. Taji
B. Uvoo
C. Kibanio
D. Hina

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswili 31-40**

Matokeo ya mtihani wa kitaifa yanapotangazwa wanafunzi waliofanya mitihani huwa wanakumbwa na kibaridi kingi kabla ya kuyaona matekeo yenyewe. Si kuwa wanaogopa kuanguka, bali pia hali ya kutokuwa na uhakika na kile watakachotuzwa baada ya muda huo wote wa kupirikana na masomo.

Mtihani wa mwaka jana ulipotangazwa, Gange ndiye aliyekuwa ameibuka mshindi shuleni kwao, kwa kupata alama magana manne na sitini katika jumla ya alama zote mia tano. Msimu huo wote alijawa na mseto wa furaha na wasi wasi. Alifurahi kwa kumaliza masomo ya msingi na sasa angeelekea katika shule ya upili. Katika masomo haya, alikuwa ameruka viunzi si kidigi; njaa, uhaba wa vifaa muhimu masomoni ikiwemo vitabu na hata sare.

Kwa upande mwingine alikuwa na wasiwasi wa mwasi kisa na maana, angegeuzaje ukurasa huo na kufungua, ule mwingine. Ilikuwa ibada kwake, kwani huo mmoja usingemkidhi kwa vyovyote vile. Angefungua mwingine na mwingine hadi kisa chote cha masomo kikamilike.

Nakumbuka vyema magharibi hiyo alivyoketi chini ya mwembe. Mkononi alikuwa ameshika bahasha ambayo ilikuwa na barua ya mwaliko wake wa kujiunga na shule ya upili. Mawazo yalimzunguka kama tiara iliyorushwa angani. Alishusha Pumzi alipokumbuka namna alivyo kamilisha masomo ya msingi kwa muujiza wa kipekee.

Alimkumbuka rafiki yake aliyefanya mtihani huo kutokana na shinikizo la wazazi pasi na hiari ya moyo. Jina la huyu barubaru lilikuwa Hainge. Kijijini Hainge alikuwa miongoni mwa waliozaliwa katika mlango wa waliojiweza. Utajiri wa watu hawa ungedhihirishwa na viatu walivyovaa shuleni, nguo zao safi au kujulikana kwa usafi wa mazingira walimaoishi. Nyumba ya mawe aidha ilikuwa dhihirisho la utajiri. Kando na hayo, mama yao alikuwa ameajiriwa kazi nzuri.

**31.** Ni neno lipi ambalo haliwezi kuelezea hali ya mwanafunzi aliyefanya mtihani hasa matokeo yanapotangazwa.

A. Kiwewe
B. Jakamoyo
C. Husuda
D. Rangaito

**32**. Gange alifanya mtihani wake mwaka gani ikiwa mwaka huu ni wa 2018?

A. 2017
B. 1917
C. 2014
D. 2016

**33**. <u>Alikuwa ameruka viunzi si kidigi</u> kama ilivyotumika katika habari inamaanishaje.

A. Gange alikuwa mwanariadha wa kuruka viunzi
B. Alipitia changamoto nyingi
C. Alivuka vidato vya masomo
D. Alipitia madarasa mbali mbali

**34**. Ni nini kilileta mseto wa fikira za furaha na wasi wasi

A. Kukamilisha ukurasa mmoja muhimu
B. Changamoto na viunzi kibao vya kuruka
C. Ukosefu wa vifaa muhimu kama vitabu
D. Kuukamilisha ukurasa mmoja muhimu na kufungua mwingine

**35**. ………………. kama tiara ieleavyo angani kwenye upepo, hii ni fani gani ya lugha.

A. Tashbihi
B. Nahau
C. Istiara
D. Chuku

**36**. Vigezo vilivyotumiwa kupima utajiri si pamoja na?

A. Kuvaa viatu
B. Kutopiga nguo pasi
C. Kutumia magari kuenda shuleni
D. Utovu wa nidhamu

**37**. Gange alipoketi chini ya mwembe_______

A. alikuwa akitulia
B. alikuwa akicheza na bahasha
C. alikuwa akidurusu kazi yake
D. alikuwa na mawazo mengi

**38**. Ni neno gani haliwezi kutumika kama neno mlango kama lilivyotumika katika kifungu.

A. Aila
B. Kijiji
C. Familia
D. Ukoo

**39**. Kulingana na kisa tungepongeza Gange kwa methali gani?

A. Bandubandu huisha gogo
B. Mtaka cha mvunguni sharti ainame
C. Mcheza kwao hutuzwa
D. Bahati ya mwenzio usilalie mlango wazi

**40**. Mtihani alioufanya Gange

A. Ulikuwa wa kimataifa
B. Ulikuwa rahisi
C. Ulikuwa wa mwisho wa mwaka
D. Ulikuwa wa kitaifa

**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41-50**

Maajabu yanazidi kutokea kila kukicha. Vyombo vya habari hutangaza kila baya linapotokea. Mvua inapokuja huja na yake. Ukame ukija huja na yake pia. Kipupwe kikishadidi huja na yake. Juzi kulitokea ukame ulioangamiza wanadamu kwa wanyama. Mimea nayo ilinyauka na kuishia kujifia.

Hatimaye mbingu zilifunguka kwa hamaki fika. Mvua ikanyesha kidindia. Mafuriko yalizuka kama mizuka. Wengine wakakimbilia milimani. Hawakuwa salama halikadhalika walio kimbia mabondeni. Walioishi karibu na mito hawakunusurika kamwe. Kiwango cha maji kilifura si haba.wanaoishi huko ole wao. Kila mahali kukawa maji, maji yasiyo kifani.

Ajabu ni kwamba ardhi ilishiba maji hadi kukinai kukinaika. Sehemu zenye miinuko ardhi yake ilijipasua yenyewe Sehemu tambarare zilizagaa maji huku baraste zikifurika furifuri. Waama, mafuriko barabarani yaliathiri usafiri pakubwa. Wanajiolojia waliwaonya wakazi wa maeneo haya **kugura** ili kukwepa maafa hayo.

Hayo yakitokana na mvua, kiangazi nacho kilikuwa kimeteketeza sehemu kubwa ya nyika za Suswa. Aidha mlima wa Aberdares ulikuwa umeonja ndimi za moto Hayawani ambao hupatikana katika maeneo hayo walihilikiwa kwa moto huo. Nyoka na wanyama watambao waliangamia kwa kuchomwa na moto.

Wakazi wa Wanjiru waliomboleza kutokana na makali ya jua. Mifugo yao haikubahatika kwa kukosa nyasi wala maji hata meli wa jangwani hakubahatika. Wana wa waja walikonda na mwushowe wengine wao kufumwa na mvi wa manaya.

Serikali ilitangaza hali ya hatari baada ya mvua tele ya mwaka wa elfu mbili kumi na mbili. Mvua hiyo ilinikumbusha nyingine iliyonyesha mwaka wa elfu moja mia tisa tisini na saba almaarufu El Nino.

Mvua hii ilisababisha kufungwa kwa shule kutokana na mafuriko madarasani. Misala nayo pia haikuachwa nyuma. Hali ilikuwa ni hiyo hiyo. Wanafunzi wa maeneo kama vile Embu na Meru hawakuwa na njia kufika shule zao. Sehemu kama Mathare zilikuwa kama bahari.

**41**. Kwa mujibu wa taarifa, ni janga lipi haliwakumbi watu?

A. Moto
B. Mvua
C. Joto
D. Ukame

**42**. Habari za athari zinazokabili waja wa maeneo mbalimbali hupatikana kupitia vyote hivi isipokuwa.

A. Serikali
B. Redio
C. Runinga
D. Rukono

**43**. Mafuriko yalisababishwa na……….

A. Maji kujaa katika nyanda za juu na chini kutojaa
B. Kujaa kwa mito
C. Mvua isiyopungua
D. Mvua ya kidindia

**44.** Ni kina nani waliofaidika na mvua kubwa iliyonyesha.

A. Wanaoishi karibu na mito
B. Waishio mabondeni
C. Wanaoshi milimani
D. Hakuna

**45**. Athari iliyotokana na mafuriko barabarani ni ipi?

A. Ardhi kupasuka yenyewe
B. Kutatiza usafiri
C. Wanajiolojia kuonya watu
D. Kuteketeza nyasi zote

**46**. Neno **<u>gura</u>** limepigigwa kistari. Lina maana gani?

A. Hema
B. Hama
C. Chota
D. Choma

**47**. Athari kuu ya ukame inayodhihirika katika kifungu hiki ni……

A. Kuzuka kwa moto
B. Kukonda kwa binadamu
C. Kuangamia kwa wanyama wanaotambaa
D. Watu kufa baada ya kudhoofika kiafya

**48.** Meli wa jangwani ni nani kulingana kifungu

A. Punda
B. Ngombe
C. Ndovu
D. Ngamia

**49**. El Nino ilipatikana miaka mingapi kabla ya mwaka wa elfu mbili na kumi na mbili?

A. 5
B. 15
C. 105
D. 9

**50.** Ni kipi kichwa mwafaka cha habari hii?

A. Moto
B. Mvua
C. Mafuriko
D. Majanga